



REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI
THIRD ASSEMBLY-SECOND SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 15th November 2023

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

[The Speaker (Hon. Mwambire) in the Chair]

PRAYER

PAPERS LAID

**REPORT OF THE HEALTH SERVICE COMMITTEE ON THE KILIFI COUNTY COMMITTEE HEALTH
SERVICE BILL, 2023**

Hon. Ziro: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity. I beg to lay the following Paper on the Table: -

The Report of the Health Service Committee on the Kilifi County Community Health Service Bill, 2023. Thank you.

(Hon. Ziro laid the document on the Table)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

MOTION**ADOPTION OF REPORT OF THE SECTORAL COMMITTEE ON AGRICULTURE, LIVESTOCK AND FISHERIES ON THE STATUS OF NARIGP PROJECTS WITHIN KILIFI COUNTY**

Hon. Mbura: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to move the following Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Sectoral Committee on Agriculture, Livestock and Fisheries on the status of NARIGP projects within Kilifi County laid on the Table of this House on Tuesday, 24th October 2023.

I would wish to call upon hon. Mohamed to second before I give my contribution in support of the Motion.

(Hon. Mohamed seconded)

(Question proposed)

The Speaker (Hon. Mwambire): I can see that the Mover of the Motion and the Seconder both want to contribute. Okay, let me allow the Seconder because the Mover will later give his remarks.

Hon. Mohamed: Thank you, Mr. Speaker. I rise to support the Report that has been tabled and being a Member of the Committee on Agriculture, I want to kindly request this Hon. House to support the Report. The NARIGP (National Agricultural and Rural Inclusive Growth Project) project is a donor-funded project that in the first phase went through 20 wards out of the 35 wards in Kilifi County and most of these ward projects which the NARIGP has been running, we couldn't barely find something substantial compared to the amount of money that had actually been spent.

So, the Committee on Agriculture went round for sight visits to find out how the NARIGP projects have impacted the people of Kilifi. Unfortunately, we found out that the project is not the way it has been put on paper. In most of the areas that we as a Committee visited, we found out that the project was not running...because the groups that began with the projects which were funded by the beneficiaries had been disbanded because of what they called the cost of the project to proceed.

We visited several groups including poultry, beekeeping, and livestock and then there was one that we visited in Chonyi which was a landslide. They are making trenches to avoid soil erosion, so basically the Committee findings...

The Speaker (Hon. Mwambire): Maybe for the benefit of Members where is Chonyi?

Hon. Mohamed: It is in Mwarakaya, sorry, it is in Junju Ward that is where we went and at least this one component had succeeded because the trenches had been done well and we could find trees in the areas where they had avoided the soil erosion. Component one which was basically more on poultry farming, most of our farmers who have been funded Kshs500,000 because it is Kshs499,999 you can easily round off this figure.

Most of these farmers had no chicken by the time we visited and when you ask them, they will tell you that they were informed that they had been funded Kshs500,000 from the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

NARIGP Project but then they were supposed to receive...because they did not receive money in cash from the group side. Money was being disbursed to an account called CDS account and this was a ward-formed committee which was supposed to take care of the funded amount. The items that they were supposed to receive they did not either receive fully or they did not receive at all.

I have a case in Bamba Ward where the group was awarded Kshs500,000 but then the items which that group was supposed to receive were given to another group. So, the group had to do their 10 per cent input, which was a requirement in the project but then the rest of the NARIGP items which they were supposed to benefit from, they did not actually receive them. Upon asking the extension officer, a week before they knew we were to visit the area, they had visited the group, and they informed the group that they were going to receive items a week after we had visited. I am not sure even by now if that group has received the items they are supposed to receive.

The second group still in Bamba, we found that it had received an award of Kshs200,000 but they were given less than what they were supposed to receive. They were given I think some iron sheets, a tank, and a few items which they could not even construct the building in which they were supposed to put the chicken. So, this was not in Bamba only; there were some other areas where we found that most of the items which were supposed to benefit the group Members... because I understand now the project is moving to phase two and in that, the 20 wards that have benefited from the first phase are now upgraded to cooperatives.

Unfortunately, we are upgrading to cooperatives and groups which do not exist because they have been disbanded; the farmers are taking care of the chicken at a personal level which was the aim of the project but it was wrongly achieved. The Committee found that there was something that went wrong which is why we called all the Chairpersons of the CDDC Account to this Assembly. We also called the Committee on Procurement Finance and the overall Chairperson, and they all came.

Hon. Members, even if you are not a Member of the Agriculture Committee you could see the Assembly was full on that day; we had to take other people to the gallery. We needed to know what happened. We found out that these people had been pushed because the training that was given was for only three days on the procurement committees. These committees were taken for training for only three days and were told you go and work; anything that you cannot do we will assist you.

The base of the project was that it benefits the common *wananchi* at the ward level. Even the tenders were supposed to be given to local suppliers. Unfortunately, most of these items were not supplied by the local suppliers because the CDDC procurement committees were instructed from *up*, that is what they told us, and we found out that *up* meant the County Procurement office. It is the plea of the committee...

The Speaker (Hon. Mwambire): Was it from the authorities or from up?

Hon. Mohamed: They said from *up*, but we understood it was from the authorities because they were told after the training that if there is anything they cannot deal with they will be assisted. So, that means it was the County Procurement office. By assisting it was giving them direction...

The Speaker (Hon. Mwambire): Next time the committees will have a dictionary for Members to know the meaning of different words.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Mohamed: So, the Committee found out there was something wrong at the County level. I believe every Member has a copy of this and there are several recommendations that this Committee has made. We found that this is a donor project, and it is out in the public; the audit was done and Kilifi was performing well according to documentation.

When you go to the ground, I believe many other Members here managed to get the first phase; they can attest from their Wards how the NARIGP project has performed. We found out that it did not perform so well among many other recommendations. I will pick one because other Members are here, and they will also pick one.

We were requesting this hon. House that because there were so many misplacements of priorities of the project objectives, we wish this House to concur with us and support us in this Report. That, the County Project Coordinator, the County Project Accountant, the County Project Procurement Officers, and the head of component one which is the poultry to be precise, to be removed from the project. They should not proceed with the second phase because if we do, then the same in the first phase might happen. That is why we want to caution and request this House to support us on that. I stand to support the Report and wish to appeal to my fellow Members in the House to support the Report.

AMENDMENTS TO THE MOTION

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. I beg to move an amendment to the Motion. I beg to move that the Motion be amended as follows: -

THAT, Recommendation six be amended by inserting the phrase “going forward” between the words “That” and “The” to read: That going forward the project coordinator should ensure monitoring and evaluation of the project and provision of quarterly Reports of the progress on the project to be submitted to the County Assembly through the Department.

Amendment number two, is on recommendation number seven which reads, “the County Project Coordinator, the County Project Accountant, the County Project Procurement Officer and head of component one be removed from the project.” My amendment is that recommendation seven be amended by adding the following phrase, “paving way for investigations by relevant authorities” after the word “project”. It should read “That the County Project Coordinator, the County Project Accountant, the County Project Procurement Officer and head of component one be removed from the project paving the way for investigation by the relevant authorities”.

Thank you, Mr. Speaker. I call upon hon. Ziro to second the amendment.

Hon. Ziro: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I second the amendment to the Motion.

(Question of the amendment proposed)

Hon. Kubo: Asante sana Bw. Spika kwa nafasi hii. Kwanza, nikiwa mmoja wa Kamati hii ya Kilimo, nasimama kuunga mkono Ripoti hii. Kuna kitu ninapinga na ni swala la kwamba watolewa ili kufanywe uchunguzi. Sababu ya kupinga ni hii; huu ni mradi wa shirika lisilokuwa la kiserikali na mambo yakichunguzwa watakuwa *exposed*. Na huyo mfidhili anaweza simamisha mradi huo unaosaidia mkaazi wa Kilifi ...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Ngirani.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Ngirani: Mr. Speaker, the point to be taken home is that the NARIGP project is over. Actually, we are shifting to another project by the name National Agricultural Value Chain Development Project. So, paving the way for investigation is about the project that is over the NARIGP project. So as a House, our job is to oversee and if we allow corruption to continue, then even the second project will not instill confidence in these donors, Mr. Speaker. Thank you.

The Speaker (Hon. Mwambire): Proceed, hon. Member.

Hon. Kubo: Nasimama kuunga mkono Hoja hii. Na nikiendelea...

The Speaker (Hon. Mwambire): Sasa, saa hii tunaunga mkono mapendekezo ya mabadiliko?

Hon. Kubo: Ninapinga mabadiliko.

The Speaker (Hon. Mwambire): Sasa ukisema unapinga hiyo ni sawa.

Hon. Kubo: Ninapinga mabadiliko kwa sababu kwamba hata kukiletwa *project* nyengine na jina lingine na bado *donors* ni wale wale wakijuwa kwamba kumefanyika ufisadi namna hii watakataa kuleta miradi mingine. Napinga kwa sababu hiyo tu. Asante sana, Bw. Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Ziro.

Hon. Ziro: Mheshimiwa Spika, wajua hili ni Bunge. Hii ni Bunge ambalo lina sheria na tuko hapa kulinda masilahi ya wakaazi wa Kilifi. Mheshimiwa aliyekuwa kwa Sakafu akisema kwamba hatuwezi tukachunguza hawa watu kwa sababu tunaogopa kwamba huenda wafadhili wengine wakose kuja Kilifi, mimi naona atakuwa anapotosha hili Bunge kwa sababu tayari ule mradi ambao umekuwa awali kama Naibu Mwenyekiti ameweza kuelezea Bunge hii kwamba huu Mradi haujanufaisha wakaazi wa Kilifi na ni mamilioni ya pesa ambayo yametumika na wale wafadhili kufikia sasa wanajua kwamba kuna wakaazi wengi wa Kilifi ambao wameweza kunufaika.

Kwa hivyo, nafikiri hakuna cha kuogopa, mheshimiwa Kubo, hapa ni hawa watu wapelekwe kule waweze kuchunguzwa na tujue ukweli uko wapi na wakipatikana na hatia sheria iweze kuchukua mkondo wake. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, you should know that you are now contributing to the proposed amendments from hon. Ngirani. So, if you stand, you indicate whether you support the amendments or you do not support the amendments and thereafter, we are going to take a vote on the same. Hon. Mbura.

Hon. Mbura: Mr. Speaker, I want to make it very clear before this House that we are here as hon. Members to execute the very important role of overseeing the projects within our county and if we become cowards of the investors yet we misuse our resources, it means that we are not ready to bring change to the masses that are within our county in implementing such projects as NARIGP. We should stand as an oversight team to ensure everything goes within what is stipulated in the project document so that at the end of the day, we achieve the objective of the project and again the lives of our people that were targeted also improve.

I therefore stand to support the amendment and I want also to urge my hon. Member Kubo being a Member of the Agriculture Committee, I think this House depends on our findings and observations and our decision towards the same because we are the people or hon. Members who went to the field and saw what happened. So, I am wondering *mheshimiwa* at this hour you are rejecting an amendment...

The Speaker (Hon. Mwambire): It is his democratic right, so convince him.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Mbura: I request the other Members to support this amendment because it is important in this programme and even in other programmes within the Agriculture Department. Thank you.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Elina Mapenzi.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii. Mimi naongea kama mwanakamati na naamini kila mwanakamati ana uwezo wa utendaji kazi. Sisi tulitembea Kilifi hii kuangalia maswala ya NARIGP vile yalivyokuwa yanakwenda. Hayajakwenda kwa ukamilifu na tulifikia hatua ya kuandika Ripoti kukaa kujadiliana kama Kamati na tukaja na mapendekezo na hadi tukakubaliana Ripoti ile ambayo sasa iko kwa Meza. Ikiwa kulikuwa na mabadiliko, mimi mwanzo kwangu ni ghafla na siwezi kwenda kinyume na mapendekezo ambayo tuliyafanya kama Kamati na sijayaona na mapungufu na hakuna aliyenijulisha kuna mapungufu ya hiyo Ripoti. Mimi napinga hayo mabadiliko ya mheshimiwa Ngirani; ninaomba tujadili Ripoti kama vile ilivyotoka kule kwa Kamati. Kwa hivyo ninapinga, Bw. Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Rafiki.

Hon. Rafiki: Asante, mheshimiwa Spika. Mimi pia ni mwanakamati katika Kamati hii ya Ukulima na tulipopata fursa ya kuenda kule mashinani kuona wale wananchi vile walivyofaidika na huu mradi, nasimama hapa nikisema kwamba ni jambo la kusikitisha kwamba maafisa wahusika wa kusimamia mradi huu waliwahadaa wale wananchi. Na ili liwe funzo, kwa sababu inaonekana ni kama ni tabia ya kwamba watu watumie pesa za umma vile wanavyotaka wao na waachiliwe watembe vile wanavyotaka.

Kwa hivyo, mimi nimesimama kuunga mkono hayo mabadiliko kwamba wale watu wachunguzwe wakipatikana na hatia wawacheni washtakiwe wawe mfano kwamba pesa za umma zina haki ya kulindwa. Kwa sababu hizi pesa pia ni pesa za wafadhili hata wale wafadhili wataridhika kwamba wakati wakileta pesa zao Kilifi zikitumiwa vibaya wahusika wanachukuliwa hatua; itajenga jina kwa Kaunti ya Kilifi. Asante, mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Shehe.

Hon. Sheshe: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii na kuangalia mageuzo yaliyofanywa na kiongozi ambaye alitaja herufi fulani kwamba ziwe zitabadilishwa na kuongezewa uzito.

Mimi Bwana Spika, nina uhakika wa kusema kwamba kazi waliyoifanya Kamati hii yetu walifanya kazi nzuri na kazi nzuri waliyoifanya kadri ya mmoja baada ya mwengine anayesimama hapa kupeana mawazo yake, tumekuja kugundua kwamba kutoka nambari moja mpaka saba majibu haya yako kidogo maji maji; hayana uzito katika huu mradi wa bilioni ukiangalia shilingi bilioni moja tukiwa tunazungumza habari ya Kaunti ya Kilifi iliyo na waheshimiwa. Ningeomba kwa unyenyekevu mheshimiwa Spika, hili karatasi lirudishwe katika kitengo chetu cha sheria waende wakaangalie ule uzito wake wa kupoteza heshima yetu na pesa za mfadhili majibu haya hayaendi sawa na vile wameweka hapa hii bado iko maji maji kwa sababu itatuonyesha kwamba sisi tunashirikiana ...

The Speaker (Hon. Mwambire): Sasa mheshimiwa, kuna mheshimiwa Ngirani ameleta mapendekezo ya kufanya mabadiliko ya hii sehemu ya sita na ya saba ili ziwe na uzito zaidi kulingana na vile walikuwa wanasema. Ndio wewe unaunga mkono yale mabadiliko ambayo yamewekwa ama huungi mkono?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Shehe: Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni wazo jema kwa mheshimiwa Ngirani lakini bado iko maji maji; inataka uzito zaidi. Kwa hivyo, mimi nayapinga kabisa. Napinga hayo aliyobadilisha ili tumpatie nafasi mwanasheria atupatie mwelekeo. Asante.

Hon. Brown: Asante, mheshimiwa Spika. Naunga mkono mabadiliko yaliyofanywa na mheshimiwa Ngirani kwa sababu tano ambazo nitazitoa.

Sababu ya kwanza, tunashukuru kwanza kwa sababu ya huu mradi ulioletwa kwa ajili ya kunufaisha wananchi wetu hapa Kilifi. Ni jambo la kushukuru Mungu kwa sababu alitutunuku kuona kwamba hapa Kilifi yule mwananchi wa chini ambaye amebadilishwa jina, amebandikwa jina kuwa *hustler* nafikiri atabanduka kutoka kule ku-*hustle* na atakuwa mtu anayepata mapato. Hii ni shukrani ya kwanza.

Jambo la pili, ningelipenda kuzungumza maswala ya Bunge letu; ndugu zangu tujue kwamba kazi tunayoifanya ni kazi ya kumlinda mwananchi na raslimali zetu. Hata tukiangalia maandiko kwa Bibilia yanasema kwamba yule muoga haingii mbinguni. Si kwamba ufanye dhambi, ukiwa wewe ni muoga tayari hutaona ufalme wa Mungu.

(Laughter)

Kwa hivyo, inashangaza kwamba sisi tukiwa hapa Bunge watu ambao ni watunzi wa sheria na pia kuhakikisha kwamba sheria hizi tutajaribu kuona kwamba wananchi wetu wanapata afueni.

Jambo la tatu nasema hivi. Mimi ni shahidi katika sehemu yangu ya Mtepeni kwa hali ya utapeli ambao uko pale. Haiwezekani kwamba sisi tumejenga kibanda halafu unaambiwa kwamba kibanda kiko, halafu kile kibanda unaambiwa kimewekewa pesa fulani. Hizo pesa zinazungumzwa zimeonekana na Kamati kwamba hizi ndio pesa zimewekwa na kule mashinani sivyo ilivyo. Hii ni hatia kubwa sana. Tukisema kwamba sisi wabunge tutalalia masikio na tuseme kwamba wacha haya yaendeleo, haitakuwa sawa.

Jambo lengine ningependa kuzungumza hapa ni kwamba napongeza kazi ambayo Kamati iliifanya. Mlifanya kazi kubwa ambayo tunaipigia upatu; kwamba pongezi na kongole Bw. Mwenyekiti kwa sababu kazi hii mliyofanya ni kazi ya maana. Lakini, mheshimiwa Ngirani kwa sababu ametimiza jukumu la sisi, kazi yetu iliyoko hapa ni kwamba kuongezea kwamba haina maana ati unamtoa unamuweka kando, umefanya nini? Kama una chawa ama kunguni lazima udondolewe ili uwe safi na kama utakuwa safi utaregeshwa tena kazini, lakini useme tutoe tuweke kando bila matibabu hakuna kitu tutakuwa tunafanya ndani ya Bunge hili.

La mwisho, naunga mkono kwa dhati mageuzi haya na ningelipenda kumuunga mkono zaidi mheshimiwa wetu ambaye alikuwa kwa Sakafu kwamba ingeongezewa uzito zaidi hata wakipatikana na hatia wawekwe ndani kabisa lakini nafikiri yeye kwa sababu sisi si wanasheria ndio alikuwa anajaribu ku-*refer* kwamba hiyo ingeongezwa ili wale wanasheria ama ingekuja hata kwa Kamati yangu ya Haki na Sheria tukajaribu kuichonga vizuri na tukaongezea ile ambayo inastahili.

Asante, Bw. Spika kwa kunipatia fursa hii ya kuzungumza Hoja zangu kwa ajili ya Kaunti yetu ya Kilifi.

The Speaker (Hon. Mwambire): Labda hii ya saba ukiangalia vizuri vile imeandikwa iko sawa na Biblia; inasema asiyefanya kazi asile. Na ikisema asiyefanya kazi asile, kama hutakula?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Biblia haikukamilisha hapo. Kumaanisha utakufa! Kwa hivyo, hii nayo inasema ipeane nafasi ya kuchunguzwa. Mheshimiwa Morris Kitsao (Hinzano).

Hon. Hinzano: Asante, mheshimiwa Spika. Nasimama kuunga mkono marekebisho yaliyoletwa na Mheshimiwa Ngirani asilimia 100. Naunga mkono kwa sababu zifuatazo; Kaunti yetu ya Kilifi hali ya umaskini umezidi sio kwa sababu hakuna raslimali ama hakuna mipangilio mizuri ya wananchi maisha yao kubadilika bali ni kwa sababu wale ambao wanakuwa kwa maofisi wamegeuza zile ofisi kama ni mali yao na sio mali ya wananchi.

Nafananisha shirika hili na wale wasimamizi haswa wasimamizi, nawafafanisha na Riwaya moja ya 'Masaibu ya Ndugu Jero'. Ni riwaya ambayo ndugu Jero alikuwa ni mtumishi wa Mungu lakini alikuwa lengo lake kuu sio kumtumikia Mungu maanake, alikuwa ana kibanda amejenga katika ufuo wa bahari na lengo lake ni kukusanya sadaka na kuiba bibi za watu usiku.

Hawa sasa ni wale wasimamizi wa huu mradi ikiwa hilo shirika lilikuwa na nia njema lakini hawa wamegeuza kwamba wananchi wanawatumia tu kama kigezo kwamba fedha zimefikia wananchi pale mashinani lakini sivyo. Ni kwamba, kuna mpango hata katika wadi yangu ya Kakuyuni kuna makundi zaidi ya saba ambayo yalinufaika, lakini sasa hivi wale wanachama wote hali zao ni maskini hata kuliko vile walikutwa wakati wa mwanzo. Walipatiwa ahadi na mipangilio ambayo sio ambayo iko kwa sababu kwa sasa hivi katika yale makundi, utakuta wanatufuata wengine wakiomba msaada angalau waweze kujikwamua ilhali fedha zililetwa kwa ajili ya huu mradi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yatatoa funzo kwa wale ambao wataingia katika hiyo ofisi na kumuomba tu mheshimiwa Kubo kwamba katika Bunge hili, mwananchi hana utetezi wowote isipokuwa wewe ambaye umefika katika Bunge hili. Hapa sio mambo ya kuangalia mtu mmoja ambaye yuko kwa ofisi; ikiwa yuko kwa ofisi na utendajikazi wake ni mzuri ni sawa lakini ikiwa utendaji kazi wake unadhuru wananchi huyo mtu ni haki atoke na vitengo maalum ambavyo vinahusika na mambo ya uchunguzi vifanye uchunguzi na sheria ichukuliwe. Hatujasema kwamba ana makosa ama hana.

Katika mambo mengi sana ya viongozi huwa mara nyingi tunajisahau kule tumetoka kwamba ni nani tunamshughulikia; tunamshughulikia mwananchi ambaye hana utetezi wowote, sauti yake ni wewe ambaye umetumwa katika Bunge hili ili kuweza kumtetea. Nasimama kusema kwamba hatua ichukuliwe na sasa hivi ikiwezekana hata kwa hizo ofisi waweze kutoka mapema ili uchunguzi ufanywe, ili hatua ichukuliwe na iwe ni mfano hata kwa wengine. Sio kwa shirika hili pekee bali kuna mashirika mengi sana na kama Bunge pia tutakuwa na mpangilio mzuri.

Kuna mashirika ambayo ni ya ndani ya nchi ambayo yanadhulumu wananchi vibaya sana hususan haya mashirika ya kukopesha vijana pikipiki. Wananchi wanalipa kwa bei kubwa; mara tatu, ilhali ikiwa hata bado pesa kidogo kama shilingi elfu 20 pikipiki inachukuliwa na yeye amelipa zaidi ya laki mbili, lakini pikipiki inaenda anarudi kuwa maskini.

Kwa hivyo, kama Bunge lazima tuweke mipango ya kumtetea mwananchi maanake mwananchi anaumia na hakuna mwengine anaweza kumtetea isipokuwa sisi ambao tumetumwa katika Bunge hili kuweza kufanya utetezi. Asanteni sana kwa mchango huo, na naunga mkono marekebisho hayo.

Hon. (Ms.) Mariam: Asante, sana Bw. Spika. Nasimama kuunga mkono mabadiliko yaliyoletwa na Mheshimiwa Ngirani haswa hili la kuwa hawa wako kwenye maofisi wakae kando, wachunguzwe wakipatikana na hatia hatua ifuate mkondo wake na ikiwa hawana hatia

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

basi waregeshwe. Mnenenaji aliyetoka, amesema kule kwake Kakuyuni kuna makundi ambayo ilibidi wanaomba omba kupata chakula cha wale kuku; mimi ni mmoja ambao nishatoa pesa zangu katika maswala haya.

Ukiangalia ule mradi ulikuwa umepangwa hali ya kuwa wataletewa hao vifaranga na kuna chakula pia watapewa. Lakini ilifikia mahali hata wale wakulima walikuwa chakula hawakipati. Kamati ilipotembelea labda kuna makundi mliona walipewa kuku kama hamsini lakini wengine wakafa kwa sababu wale wananchi hawawezi kumudu lishe ya wale kuku. Huu mradi ulikuwa kamili kabisa na hakufanywa hapa Kilifi Kaunti peke yake. Mradi huu uko kwa kaunti nyengine na umefaulu vizuri sana.

Bw. Spika, sisi kama Kaunti ya Kilifi hatuko vizuri kwa maswala ya ufasidi. Tukiangalia hata vile jana Gavana alivyoitwa kule Seneti alivyoitwa...

(Hon. Rafiki stood on a Point of Order)

Hon. Rafiki: Asante, mheshimiwa Spika. Ningeomba mheshimiwa aliye kwenye Sakafu anieleze vizuri nielewe. Hatuko vizuri upande wa kiufisadi kama kaunti ki vipi? Ni tuongeze ufasidi zaidi ama hicho Kiswahili...

Hon. (Ms.) Mariam: Nimekuelewa. Yaani labda Kiswahili kimenipiga chenga kiasi lakini nilikuwa namaanisha yakizungumziwa maswala ya ufasidi hapa Kenya, sisi Kilifi tuko ndani zaidi. Ikiwa kuna watu walifwatilia mazungumzo jana ya Seneti ilikuwa ni aibu kubwa sana. Kuna watu walikuwa wanauliza *County Assembly* ilikuwa wapi mpaka tufikie huko? Sisi ndio tuna jukumu la kuhakikisha kwamba mambo kama hayo hayafiki kule. Sisi ndio watu wa kwanza kuangalia mali ya umma inatumika vizuri. Ikiwa tutakuwa na uoga wa kufuatilia aidha ni watu wa upande wa serikali ama pesa zimekuja na wafadhili, kwa sababu pesa hata zikija na wafadhili lengo lake ni kuwa yule mwananchi afaidike. Kwa hivyo, zinakuwa ni pesa za umma.

Sisi ndio tuna jukumu la kuhakikisha tunalinda zile pesa za umma na lazima ziwafaidishe. Kwa hivyo, Bw. Spika, kitu ambacho natilia mkazo ni kuwa sisi tuko na majukumu na lazima tuyafanye kulingana na sheria ilivyotupa nguvu ili hata ikiwa tutatoka katika Bunge hii, wananchi wajue hili Bunge limewatetea wakapata haki yao, limelinda raslimali zote za hii Kaunti kwa sababu hiyo ndio kazi yetu. Ikiwa hatuwezi kufanya kazi hiyo basi hatuna faida ya kuwa katika Bunge hii. Kwa hivyo, naunga mkono mabadiliko yaliyoletwa na Mheshimiwa Ngirani. Asante.

Hon. Tete: Asante, Bw. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Nataka nitumie nafasi hii kama wananchi wa Shimo la Tewa jinsi walivyonituma niwawakilishe. Nachukua nafasi hii nikiungana na wana Kilifi wote nikisema haki zao zazama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mabadiliko yaliyoletwa na Mheshimiwa Ngirani kwa sababu moja ama nyingine ni kwamba Kaunti yetu ya Kilifi ina matajiri wachache sana walioweza hwa na utawala mbaya wa ugatuzi wa miaka kumi iliyopita. Watu ambao walipora mali ya umma kwenda kujiwezesha hao wananchi wakilia njaa hali haki ilikuwa imewalenga.

Ninawafananisha hawa watu na mwanamke mmoja ambaye alipata bwana aliyekuwa na uwezo akifanya na mahoteli. Walikuwa wanaleta vyakula aina tofauti tofauti lakini hali ilipokuwa mbaya ikawa chakula kinapatikana kwa dhiki. Mfano wake ni kama wakati wa Corona. Siku moja mwanamke huyu akatembelewa na mamake vyaa. Alipofika pale akampigia mumewe akamwambia huku kuna mgeni. Mgeni gani? Akasema mama amefika. Akaulizwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mamako wewe ama mamangu mimi? Akasema mamako wewe. Akasema sawa. Akasema wasemaje sasa. Tuma pesa nikanunue samaki nataka leo ale vizuri; nitampikia ajue ako na mkaza mwana wa kumthamini.

Mheshimiwa Spika, mume akafanya hivyo akijua ya kwamba mamake leo atakula vyema kwa sababu ameisikia sauti ya mkewe ya kwamba anataka kumuandalia vizuri. Pesa zikatumwa za kwenda kununua samaki na kila kitu mpishi angehitaji. Pesa zilipoingia, mwanamke akasema hata mimi za matumizi sipewi lakini mama akifika ninaweza kupewa elfu nikanunue samaki? Akatoa mia mbili akanunua pojo na nazi. Mume alipotoka kazini akiwa na furaha kumuuliza mamake. Alisema nashukuru hizi pojo nilikuwa nimezipeza kitambo. Nimepikiwa pojo vizuri sana na mkaza mwanangu. Yule Bwana akasema, sikutuma pesa za pojo mimi, nimetuma pesa za kwamba ule samaki. Akamwita yule mke na akamuuliza umempikia mama nini? Akasema nimezunguka lakini nikaona nitampikia kesho.

Huu msemu nauzungumza kwa sababu gani? Wananchi wanadhulumika na sisi ambao tunategemewa na wananchi kuja kuwatetea na ni sisi tunatafuta njia kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanasalimika. Umaskini umetanda ndani ya Kaunti ya Kilifi na pesa zinazama zile ambazo ni zetu sisi. Hatuwezi kuzisimamia na tukauliza kwa nini watu wetu wako hivi? Zimetoka kwa watu wanaleta pesa za misaada wakisema wacha tuangalie wale watu watasaidikia namna gani. Bado twarudi pale pa kusema kwamba kusimamia hilo jambo nalo ni shida. Tuliletwa kwa kazi gani hapa kama huwezi simama kutetea mwananchi ambaye amekutuma hapa ili apate ile haki ambayo anajua nimetuma mtu wa kunitetea.

Kuna mzee fulani mahali alikuwa anasema mtu ambaye hawezi tetea mtu ni afe, na alikuwa anapenda sana kusema huu msemu huwa namchukulia ni kama anazungumza mzaha mitaani. Lakini wananchi wanatutazama. Leo tumepata watu wameangaliwa katika Bunge letu, Kamati imeenda nje na ikaona kuna udhalimu na mwananchi anapotezewa haki zake; sisi tunasema kwamba mfidhili hatakuja tena. Kabla aje mwananchi anaumia. Amekuja ili mwananchi afaidike wewe unasema hatakuja tena kwa hivyo unataka aje kwa sababu ya watu watatu? Wananchi wote waumie sababu yako? Kama ni kukosa afadhali akose yeye ambaye amelengwa na huyu ambaye anajua kupika pojo na kunyanyasa wenzake akose kila kitu. Kwa hivyo, nasema kwamba Mheshimiwa Ngirani hongera sana na ninaunga mkono kama kungekuwa na sehemu ya kuongezea makali, ingewekwa. Huu si wakati wa kucheza na tuangalie mali za wananchi zinazama. Wewe wapata hapa kile unachopata lakini ukipeleka kule hakikutoshi na wewe mwenyewe ni shahidi. Wakati mwengine hata unatafuta nyumba ya kupangisha nje kwa sababu unajua ukifika kule waombwaombwa.

Angalikuwa amepata huu mradi na anajitegemea angekuomba kweli? Kwa hivyo, huu ni wakati wa kuangalia mwananchi atatetewa namna gani. Tukianza kusema ya kwamba hatakuja hatakuja, sasa akija anakuja wapi? Aje azulumiwe tena? Hayo mambo tuache. Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, huu ni wakati wa kuangalia haki iwe haki.

Mimi sioni kama watatoboa hawa, kama mambo ni haya ambayo tumeyapata hapa. Wataenda wakienda tu! Na kama kuna wafuasi ambao walirambishwa hapa waseme ya kwamba tumerambishwa kwa hivyo tuna sababu ya kutetea. Kutoka hapa kamwambie ya kwamba nimejaribu lakini nimeshindwa; wengi wamesimama upande mmoja wa kutetea mwananchi. Mimi nimesimama hapa kusema ya kwamba tunaendelea...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is a point of intervention.

Hon. Tete: Hata mwenye *intervention* amechelewa!

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Mapenzi: *Sijachelewa!* Hon. Speaker, we are in a House of Order and decorum. So I request the Member on the Floor to withdraw the word or apologize before this House the word “*Kurambishwa*.” First, he should explain it to us, we understand it, because the meaning of which we know it, is not something one should appreciate whenever they have been told in that category. So, please the Member on the Floor; explain to us what is “*kurambishwa*” and then you apologize and withdraw it.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Tete, I think it is good to use Parliamentary language. This is because Members in the House debate on what they understand, and they have the democratic right to be on either side.

Hon. Tete: Hiyo mheshimiwa ni haki yao, hata kurambishwa pia ukitaka unachukua na ukikataa unawachana nayo. Na sijasema amerambishwa nimesema kama... Kwa hivyo kama yuko ambaye alirambishwa na ajithibitisha kwamba yeye ni mmoja lakini nimesema kama wako waliorambishwa...

The Speaker (Hon. Mwambire): Maana ya kurambishwa ndio waheshimiwa walikuwa wanataka kujua.

Hon. Tete: Maana yake ni kupewa rushwa.

The Speaker (Hon. Mwambire): Sasa hapa ndani hakuna mheshimiwa amepewa rushwa.

Hon. Tete: Kama hakuna ni vizuri.

The Speaker (Hon. Mwambire): Nafikiri hayo matamshi yatoe.

Hon. Tete: Nasemaje, Mheshimiwa Spika, wajua kuna neno ambalo ukilizungumza umelipatia nafasi ya mtu kujihoji. Ninaposema ya kwamba kama yupo ambaye alirambishwa ama alipewa rushwa basi katika Bunge hii hafai na kama hayuko sasa sote tumefanana. Tuko sote tunapiga vita vya kutaka kuona wananchi wanapata haki zao. Ukisikia mtu ana uchungu wa kuzungumziwa mambo ya rushwa labda...

(Hon. Mapenzi stood on a Point of Information)

Hon. (Ms.) Mapenzi: Mheshimiwa aliye kwa Sakafu naomba uketi nikueleze vitu.

Hon. Tete: Nieleze.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Hapa tuko katika majadiliano yenye uadilifu; hatuko hapa kulumbana. Kila mmoja ana haki ya kusimama upande ambao amejichagulia na isiwe ni sababu ya wewe kuwaekeza katika viwango ambavyo hawahusiki kwamba wao waliopinga huenda wamekula hongo. Nataka ieleweke katika hii Bunge na nje ya Bunge hii kwamba hakuna hongo imechukuliwa ni kila mmoja anasimama katika demokrasia ya kuchagua ni upande gani atasimama. Kuendelea kujadili kwa namna hiyo unakosea heshima Bunge hii; unakosea heshima wale wenzako ambao wamesimama kujadili hili swala kwa upande wa kupinga. Ninaomba uombe msamaha na uendele na maongezi yenye uadilifu.

The Speaker (Hon. Mwambire): There is another intervention from hon. Ziro.

Hon. Ziro: Asante sana, mheshimiwa Spika. Mimi ninaona ambacho Mheshimiwa Tete ameongea kwa ujumla na hakuongea kwa kutaja mtu fulani katika hii Bunge. Nafikiri amefanya hivyo kwa sababu alijua ni Bunge ambalo ni la kupewa heshima yake.

Kwa hivyo, naona kutakuwa kuna utata kidogo tukiona ameanza kuingiliwa. Mheshimiwa Tete, nafikiri ameongea na akatoa hisia zake, na ninaona ameongea kwa uchungu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

sana. Ameongea kwa uchungu kwa sababu hatungetaka kuona hizi mali za wananchi ambazo zimepotea zinaenda tu bila kujulikana zinaenda vipi.

Mimi sioni kuwa itakuwa na haja kwa mheshimiwa Tete kuomba msamaha kwa kuongea kitu ambacho ni sawa ni vile tu amekiongea akiwa na hisia akiweza kukashifu vile vitu ambavyo vilifanywa na hawa maafisa. Asante, mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Morgan (Kubo) has an intervention.

Hon. Kubo: Asante sana, mheshimiwa Spika. Nasimama kuambia mheshimiwa aliyekuwa kwa Sakafu, mheshimiwa Ziro kwamba hii *recommendation* imeletwa leo na mheshimiwa Ngirani. Haijaletwa juzi ama jana, na tunaongea kuhusu hii *recommendation* ya leo. Kama ingekuwa kuna kitu ambacho hakiko sawa, hii Ripoti tulitembea na tukaandika na hakuna mahali ambapo tumesema kwamba hawa ambao tumewataja hapa tumewa *favour*. Tumeongea sawa, kwamba tumewaweka nje lakini haya mambo ya leo...kwa hivyo kutetea kwamba Mheshimwa Tete amesema sawa, hajasema sawa; asimame na aombe msamaha tafadhali.

The Speaker (Hon. Mwambire): *Waheshimiwa*, I have seen several interventions and counter-interventions and I think hon. (Ms.) Elina stood on a Point of Information to inform hon. Tete that whatever he was talking about... the intention. Hon. Tete had clarified that he was saying in-case. If I heard Hon. (Ms.) Elina clearly said that there is nobody "*hakuna aliyepewa hongo*" that is what she was informing Tete.

So, I think she could have stood on her ground to ask Hon. Tete to withdraw those words, but you see, she informed him that there was nobody who was given anything and now I think that we can leave it at that level because there is nobody; that is the information Hon. Tete has been given and he has not said that there is anybody.

So, I think that is very clear and it is in the record, that is why I have allowed you to share your sentiments including that information. I wish she could have stood on another Standing Order apart from the one for information.

Now, if Hon. Tete could have refused to be informed that could have been another case altogether. So, please minimize the interventions so that we can conclude this debate, vote, and then proceed as required.

Hon. Kea: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity. First and foremost, I would like to convey my message of condolences to the County Assembly of Kilifi for the loss of one of our staff, Madam Mercy Koti; may her soul rest in peace.

I want to stand and strongly support the Motion of the amendment by hon. Ngirani and I want to support this in totality. We as a House have the mandate to oversee and it has no questions; we must do it and through this, we have to stamp our authority as a County Assembly that people are not going to be allowed to embezzle funds at the expense of the common *mwananchi*.

I was following the proceeding at the Senate yesterday and if at all I can be allowed to quote the words which were used by Mr. Okiya Omtatah, Senator for Bungoma, saying that "Kilifi has a lot of resources..."

The Speaker (Hon. Mwambire): He is the honourable Senator.

Hon. Kea: Thank you! Honourable Senator Okiya Omtatah stated that Kilifi has a lot of resources, but we are living a very poor life which I was annoyed with as a Kilifi citizen. Putting these people aside and paving the way for investigation is the best way to go. Our people are

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

living in poverty not because we do not have the opportunity to better our lives, but a few individuals have decided to steal from us mercilessly.

As honourable Members, we get a lot of hard times because our people are always there asking for help. While people from outside the country have come to support us free of charge. Once you go to the ground, you meet the *mama mboga* and the very old people who are supposed to be the direct beneficiaries of this whole project or programme are living in a dilapidated state of life which is not pleasing at all. I strongly support this amendment as I again congratulate the team which did all this and came up with this Report. I stand to support.

Hon. Kalama: Thank you, Mr. Speaker Sir, for this opportunity. I stand to support the Report with the amendments for the following reasons. One, the objective of the programme was to empower the community and it has become verse versa.

Second, instead of the project being a blessing to the community, it has become a curse. So, I strongly support the amendment. Thank you, Mr. Speaker.

Hon. Munyoki: Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Nataka kuwa mmoja wa wale wanaosimama kuunga mkono mabadiliko yaliyoletwa na mhehsimiwa Ngirani. Ninazungumza na hisia kali kwa kitendo kilichofanyika. Waheshimiwa kadhaa tumekuwa tukijadili hili swala; kuna wengine wako na mashini za kuangua mayai ambazo zinasemekana zilifika mashinani na hazikufika kwa wengi. Fedha za vyakula vya wale kuku ambao walikuwa wamepewa wawafuge, walipewa magunia mawili matatu ya kuanzia ikiwa hakuna tena.

Tukiangalia, Bw. Spika, mwananchi wa chini mradi huu ulikuwa umekuja umsaidie sasa haumsaidii huku ukifaidi watu wawili watatu. Ili iwe funzo kwao na kwa miradi mingine ya wadhamini, ni vyema kuwekwe sheria kali ili vitendo kama hivi visijirudie. Kwa hayo, naunga mkono Mswada wa mabadiliko.

Hon. (Ms.) Faith: Asante, mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono kikamilifu hoja hii. Nina sababu mbili na ningependa kunukuu semi za wananchi; kama mnavyojua wananchi wakijua wewe ni mheshimiwa lazima watakupigia simu kuomba msaada. Nilipigiwa simu nikaambiwa kuku wako karibu kuzaa tusaidie na pesa ya wishwa hawana, hilo ni la kwanza.

Pia, tumejenga nyumba hatujawekewa saruji, twataka pia hiyo tutandaze ili kuku wetu wakae mahali pazuri. Kumbe miradi ni ya NARIGP ambayo wanafaa wapewa kila kitu. Kwa nini wananchi wafanywe kuwa ombaomba wakiwa walipewa mradi wa kuwasaidia ili kuwainua? Ikiwa walikuwa hawatafanyiwa vyote heri hawangewapa kuliko wawape mradi na wakose kuwapa pesa za kusimamia ule mradi. Sasa kwa sababu hiyo, mimi Mheshimiwa Faith ninaunga mkono mapendekezo yaliyowekwa na mheshimiwa Ngirani na ninaomba sheria ichukue mkondo wake kwa watu kama hawa wenye ubinafsi. Kwa nini pesa zije kufaidisha watu kidogo hapa Kilifi ikiwa sisi wote tunajua shida tulizo nazo? Ninataka uchuguzi ufanywe na ikiwa wamepatikana na hatia sheria ichukue mkondo wake. Mpaka lini tutavumilia watu wachache kama hawa kudhulumu wananchi? Naunga mkono moja kwa moja tena lifanyike kwa haraka ili wananchi wapate haki yao.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Hon. Ngirani: I want to thank the Hon. Members who have agreed to these amendments. These are meant to instill discipline in those officers who have been given the mandate to look

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

after the resources of this County. Sometime back there was a suggestion of castrating rapists. A rapist, Mr. Speaker, is not just a man who sleeps with a woman by force even those who forcefully take the resources meant for *wananchi*.

Through the Governor's manifesto and his three pillars; one of them being agriculture, the Governor who is the head of this County should suspend these people with immediate effect to pave way for the relevant authorities to do the investigation freely. They should serve as an example for those who are used to taking the resources of this County by force.

With those few remarks, I want to thank the Hon. Members for supporting these amendments.

(Question, of the amendment put and agreed to)

(Question of the Motion as amended proposed)

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, now we are reverting to the deliberations but recommendations six and seven will be as amended by hon. Ngirani so we can now proceed.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante tena, Bw. Spika, kwa fursa hii. Nimesimama kuzungumzia kuhusu swala hili la NARIGP na uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, viongozi wako mbioni kutafuta wafadhili na mashirika ya kibinafsi kusaidiana na serikali kuona vile tutakavyoinua wananchi. Swala la sisi wana Kilifi kuwa na hawa wafadhili na mashirika ya kibinafsi ni swala ambalo limelenga kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi narudi kusema nimekuwa mmoja wao wa uchunguzi wa mambo haya na labda mmoja ama wawili wamekosa kunielewa niliposimama kupinga. Sio kwamba niko upande wa kuonea wananchi...

The Speaker (Hon. Mwambire): Usiwe na hofu mheshimiwa, wewe endelea...

Hon. (Ms.) Mapenzi: Wacha niendeleo, mheshimiwa Spika. Nipe nafasi. Ninasawazisha hili maanake sikueleza kwa sababu gani napinga. Mimi nilitosheka na maamuzi tuliyoyapeana na hata kule mwisho pia tulizungumzia maafisaa hawa walioshindwa na kufwatilia uangalizi mzuri wa haya mambo ya NARIGP. Tulipendekeza watolewe katika nyadhifa zao na hiyo niliona ni adhabu tosha. Kwa kuwa wengi sasa wamesimama na kukubali kwamba uchunguzi ufanyike, mimi nitawaunga mkono maana sina sauti ya kusema isifanyike. Hili ni Bunge la walio wengi kufaulu katika uamuzi wao. Mimi niliamua hivyo kwa sababu niliona ile adhabu inatosha. Kwa kuwa Bunge limeona haitoshi, wacha pia mimi nami niwe pamoja nao.

Tulifanya uchunguzi, Bw. Spika, na kwa kweli ni kwamba kuna ulegevu wa kazi katika hili jimbo kwa maswala ya NARIGP. Udhaifu wa kwanza ni mafunzo yaliyokuwa yakipeanwa kwa washiriki wa makundi yaliyokuwa yakifadhiliwa na NARIGP; hawakuweza kupewa mafunzo ya kutosha hivyo basi jukumu la kubebana na miradi ile ambayo walikuwa wakipewa lilikuwa zito kwao ndio maana kulikuwa na mapungufu hapa na pale.

Pili, wakati Kamati zimeundwa na kuna ununuzi wa vifaa basi maswala hayo yalikuwa yanatakikana yatekelezwe na wana Kamati wenyewe. Tulibaini ya kwamba hawakuwa wanapewa hiyo fursa ya kutekeleza ununuzi wa hivi vifaa kwa sababu maafisaa walikuwa wakishiriki kwa huu ununuzi wa hivi vifaa na hivyo basi walikuwa wanawaletea vifaa ambavyo vimepungua.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mheshimiwa Spika, hata akaunti za benki zilikuwa za watu binafsi mfano ni Upendo Group; akaunti yao ilikuwa ya mtu binafsi ambapo hilo swala liliashiria kuwa ni mbinu fiche ya hizo fedha katika hilo swala zima. Zabuni hazikufwata vile ilivyokuwa yastahili. Wanakamati wenyewe ndio walikuwa wanastahili kupendekeza nani anastahili kupewa na ni kwa sababu gani. Tulivyofwatilia tulijua waliokuwa wakifanya hizi zabuni ni wale wahusika wakuu katika uongozi mzima wa NARIGP.

Mimi nasimama katika nafasi ya kusema hawa watu hawastahili kazi yoyote hapa Kaunti yetu na hawana uwezo wa kubebana na miradi ambayo itakuja hata huko mbeleni. Mradi mmoja tulikutana nao Takaungu kule Mnarani *Ward*. Tulibaini kwamba vifaa ambavyo viko pale viko mikononi mwa watu binafsi. Mradi hauendelei na wananchi tulipowauliza walisema hakuna faida wamepata. Hili si jambo zuri na hata huko mbeleni kukiwa kutakuwa na swala kama hili la NARIGP la ulegevu na ufisadi, tusimame na tupinge vikali. Tusiwe leo tunapinga hili swala halafu kesho kama ni swala lengine twagawanyana na wananchi wanaendelea kuumia. Hili Bunge tusimame kwa uadilifu na kutetea wananchi maanake walituleta hapa wakijua tumekuja kuwatetea. Kazi yetu moja ni kuwatetea.

Sauti zao zinakuja hapa kupitia kwetu na kwa kuwa wanakamati tuliwahoji na wakasema wamechoka na uongozi wa NARIGP basi wangenda mambo yabadilike na wafaidi. Nawaunga mkono waheshimiwa na kuwapongeza kwa kusimama na wananchi. Mungu awabariki na hali hii iendelee kesho tusije hapa tukazozana na swala linafanana na hili yule anaunga, yule anapinga. Vile mimi nimeungana na nyinyi, mbeleni muungane na mimi kupiga vita ufisadi na ulegevu katika jimbo letu la Kilifi. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Ziro.

Hon. Ziro: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Mimi pia nimesimama kuunga mkono Ripoti hii na nawapongeza Wanakamati wa *Agriculture* kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kufichua maovu ambayo yalifanyiwa watu wetu wa Kaunti ya Kilifi.

Katika Wadi ya Mwanamwinga madhambi haya yalifanyika. Kuna makundi ambayo yaliweza kupewa vifaranga na wakaambiwa watengeneze nyumba zao na shirika hili la NARIGP. Wasimamizi wa shirika hili hawakuwa na nia njema kwa wakazi wa Kilifi. Zaidi walikuwa wanataka wawadhulumu na kuzidisha umaskini ambao wamekuwa nao kupitia ufadhili huu.

Mheshimiwa Ngirani amependekeza waweze kutolewa na kuchunguzwa na iwapo watapatikana na hatia basi sheria ichukue mkondo wake. Kama Bunge pia, ningetaka tuweze kupata Ripoti tena baadaye kwa ule uchunguzi ambao utakuwa umefanyika. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Ngirani.

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. First, may I thank the Committee for Agriculture for this job well done. One of the missions of the World Bank is to end extreme poverty and boast of shared prosperity of a lively planet and not an individual. If donors come to a County like ours, they are here to change the lives of the people who are in poverty state.

In this Report, the reason why we have amended for these people to be investigated is because there was a total manipulation of the CDDC that is the Community Development that deals with the project on the ground by these people who were controlling this project; that is the Project Accountant, the Project Coordinator, the Procurement Officer and the Head of Component One. Groups did not receive their balances. A group was allocated Kshs500,000 and it ended up receiving less than Kshs200,000. Suppliers used to be paid without supplying the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

commodities and some supplied low-standard equipment to these groups. There was a manipulation of the procurement process. From this Report, the Community was forced by these officers to give tenders to certain companies that serve their interests and thus all this should be investigated so that we know where the truth is.

The Governor of this great county has been going on different trips to look for investors and donors. His effort must be recognized by these officers. If a donor comes in and tries to help because one of the Governor's agenda in the manifesto is to uplift the standards of his people; the standards of these people will be uplifted by the resources of this county and even the resources of donors through grants. We are here to help the Governor; we are here to oversee such projects and open where things went wrong so that the Governor can realize his manifesto. Therefore, the Governor should suspend these officers with immediate effect so that investigations can take place and uncover what has been hidden.

Mr. Speaker, we are also looking upon the Implementation Committee of this House to make sure that this Report has been implemented to the letter. The reason why we are saying these people should step aside is the World Bank is currently about to implement two projects; number one is the National Agricultural Value Chain Development Project whereby there is going to be formation of Saccos, and farmers will get loans to invest in agriculture. The same officers are said to be the ones who will monitor these projects; how if the first project of NARIGP failed miserably?

There is also another grant from the World Bank, which is the Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development Project (KEMFSED). This one is under the Blue Economy Department. If these officers are disciplined properly these projects soon will be singing prosperity.

In conclusion, for us to get more donor funds we must instill confidence in donors and one way of instilling confidence is to discipline any officer who embezzles the resources of these donors.

With those few remarks, I want to say thank you and this Report through the Implementation Committee should be implemented fully. Thank you, Mr. Speaker.

Hon. Hinzano: Asante sana, mheshimiwa Spika. Niko hapa tena kuunga mkono Ripoti hii ya Kamati ya Kilimo juu ya ugunduzi na mapendekezo ambayo waliyaleta yakiwa rasmi yamesahihishwa na Bunge ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaona manufaa ya miradi yote ambayo iko katika Kaunti yetu ya Kilifi.

Nafurahishwa na jambo moja katika nakala ya Katiba ya Afrika Kusini ambayo ina kipengee japo siwezi kukinukuu lakini nasema kwamba ukipatikana na hali kama hii ya ubadhirifu wa pesa za umma ama kosa lolote lile, tayari uko na makosa mpaka koti litakapokusafisha makosa yako. Hapa Kenya sivyo; ni kwamba hauna makosa mpaka mahakama itakapokupata na makosa.

Hichi ndicho kipengele ambacho kimweza kufanya wengi wale ambao wana uwezo kuwagandamiza wananchi kwa sababu Kamati imepata kwamba wako na makosa kwa ubadhirifu wa huu mradi ambao fedha zimetumika vibaya, lakini watakaa kwa maofisi mpaka watakapopelekwa mahakamani na maamuzi kufanywa. Huo ndio udhaifu ambao uko na kama Wabunge wa Kilifi mimi ningependekeza tu pia Kaunti yetu tuna haki ya kutunga sheria kwamba watu kama hawa waweze kuogopa na tutafanya kazi kisawasawa kuwe na sheria. Mtu akifanya kosa la ubadhirifu na kufanya maisha ya watu kuenda chini na hata wengine walipoteza

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

maisha yao kwa kuenda kwenye mradi ambao wanaufanya na hauna manufaa kwa maisha yao kwa sababu kuna watu fulani ambao wamejipanga kuwadhulumu maanake wanaona pengine hawana kauli wala uwezo wa kupeleka maoni yao ama shida zao mbele.

Kwa hivyo, naunga mkono na ikiwezekana watu kama hawa si kwa ubaya lakini wanahitaji mambo matatu kwa sababu yale mambo ambayo wanafanya yanaleta madhara hata wengine wanapoteza maisha yao. Hayo mambo matatu yakifanyika sio kwa ubaya; ni kwa sababu ya maisha ya watu wengi wameumia. Mimi maoni yangu najua katika mambo matatu hayo moja likifanyika huwa yote yamefanyika. Ukienda Mbinguni huwa umehama hapa duniani na kule pia kuna pepo na jehanam, kwa hivyo kama una makosa utaingia jehanam, yatakua yote yamekamilika. Si vizuri kuangalia mwananchi kama kitega uchumi kwa maisha ya mtu mmoja. Ni hali ambayo inasikitisha na ikiwa ni hali kama hii inaendelea inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba mwananchi anajuta kwenda kufanya maamuzi ya kufanya uongozi katika Jamhuri yetu ya Kenya, ambapo hapa Kilifi naona linaenda kuisha. Kuna watetezi ambao watawatetea, haijalishi ni madhara gani ambayo yatakuweco.

Nikiungana na mheshimiwa Ngirani juu ya mipangilio ya Gavana, ni mipangilio mizuri na hata juzi wakati anakutana na *suppliers* mimi nilimwambia watu ambao wanakufunga mikono ili kwamba mipangilio yako uliyoipanga juu ya Kaunti ya Kilifi isiende, hayo majina kama hawezi kuyafuta awalete hapa Bungeni, sisi tuna uwezo maanake sisi ndio ambao tunaisimamia sheria.

Naunga mkono Ripoti hii na itekelezwe kwa haraka na hawa watu wakiwa nje ya ofisi itakuwa vizuri zaidi maanake yule mnyonge pale ataona ameanza kutendewa haki. Asante sana, mheshimiwa Spika.

Hon. Mohamed: Asante, mheshimiwa Spika. Nasimama kuunga mkono na pia nikueleze kwamba ukiangalia mtazamo wa Bunge ni kwamba wabunge wako tayari na ningependa tuweze kusitisha mjadala, uulize swali ili tuweze kuunga mkono Mjadala huu. Asante.

Hon. Tete: Asante, kwa mara nyengine, mheshimiwa Spika, kwa kunipea nafasi hii. Chochote chema kinachofanyika kule mashinani huwa kinapatia hadhi serikali yetu pamoja na sisi viongozi na chochote kibaya kinachofanyika huwa wanasema wameanza kupatia shukrani kwa Kamati iliyoenda viwanjani na kuchunguza na kuona kwamba kuna dhulma zilizofanyika kwa wananchi. Nasema kwamba Mungu azidi kuwapa nguvu na tena mzidi kuwa wakakamavu katika majukumu hayo ambayo wananchi walitupea.

Mwananchi kule mashinani kama walivyozungumza walionitangulia wanaitwa omba omba na Mwenyezi Mungu kila mmoja anampa na wakati wake. Ilifika wakati shirika la NARIGP lilikuja kutaka kutusaidia sisi kupunguza umaskini katika gatuzi letu na zile pesa ambazo zimeletwa zilikuwa ni za kuhakikisha kwamba pale ambapo wewe ulikuwa huwezi kufika tunapata msaada. Ni masikitiko kuona ya kwamba mwananchi ambaye hangeweza kujua kilichomulenga ni kipi, lakini wewe kiongozi ama wale ambao tuliwapatia nafasi ya kwamba wawasimamie ili wasaidike hao ndio wanajichukulia nafasi za kwanza kunyanyasa wananchi.

Mahali ambapo ninasikitika napo ni hapa kwa huyu ofisaa ambaye alienda kufundishwa mpaka akaonekana anahitimu kusaidia hii jamii; hapo ndio akachukua nafasi ya kusema ni wakati wake wa kula. Kawaida hizi pesa zinapokuja mashinani, mheshimiwa kama sijakosea, huwa zinaingia kwa akaunti za wanajamii. Pesa zinapoingia kwa akaunti hizo huwa ni jukumu la wanajamii kuchagua mwanakandarasi ambaye atawapatia huduma nzuri. Kwa maajabu, ofisaa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

huyu ambaye alipendekezwa kusimamia ndiye ambaye anawachagulia *supplier* maana kwa lugha ambayo haifai wanasema washafunga *deal*.

Kile ambacho anapelekewa mwananchi ni kile ambacho akipata anasema nashukuru mimi maana hata sikuwa nacho kumbe ndiyo anagandamizwa.

Namuunga mkono mheshimiwa Ngirani alivyosema hata hao *suppliers* wachunguzwe na wakipatikana na hatia wachukuliwe hatua. Nasema hivyo kwa sababu, Kenya yetu ukifanya uovu umepatia mtu kazi.

Mheshimiwa Hinzano amesema kwamba mwizi amejulikana badala achukuliwe hatua Kenya hii, mpaka kutengenezwe Tume ichunguze kama ameiba kweli. Mapungufu tumeyaona, mheshimiwa Spika, kwamba kuna vitu vimepotea. Kama ni *tray* hamsini (50) zilikuwa zinunuliwe na zimenunuliwa ishirini (20) si tutajua thelathini (30) zimeibiwa. Naomba Gavana asichelewe kuchukua hatua ya kuona hawa wafanyakazi ambao wanatumia vibaya rasilimali za wana Kilifi wamewekwa pembeni na hatua za sheria zichukuliwe.

Mimi nitafurahi na nitashukuru nikiona kwamba yule mwananchi wa kawaida akiumia lakini anayemuamiza naye ana haki yake ameipata ya kisheria. Ninaunga mkono mageuzi haya yaliyofanyika yakifatwa na utendaji kazi ya Kamati ya *Implementation*. Chukueni hatua ya haraka ili mwananchi ajue kwamba kuja kwetu hapa kuna afueni ya kuwa tunawatetea. Hata kama hatutafikia mahali ambapo wanatarajia lakini wapate matumaini angalau asilimia sabini (70) ama themanini (80). Asante kwa kunipatia hii nafasi, na waheshimiwa wenzangu naona twaendelea vizuri sasa sauti imekuwa moja na tuzidi kusimama kwa kauli moja ili tuzidi kutetea wanachi wetu. Asante sana, mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Mbura, please respond as the Mover.

Hon. Mbura: Thank you, Mr. Speaker, for this opportunity to be able to respond to the Motion before this House. I request you to allow me to give a very brief narration.

The Speaker (Hon. Mwambire): No, just respond to what the Members have said because they have read and understood and now want to take a vote because there are no contradictions.

Hon. Mbura: I first want to thank Hon. Ngirani for bringing this Motion of amendments and thank the Members for their support to this Motion and further adopting it. Whatever has been said here is in the Report, let me thank the Committee Members of Agriculture for the tiresome job they did. This is a unique approach used by the Members. We were able to meet the beneficiaries in the field, a few suppliers, the Chairperson of the CDDC and the Executive team at the Assembly. The observations and findings rhymed with the ones we found in the field.

I stand to support this Report with amendments, and I insist the implementation team fasten this recommendation to be implemented as soon as possible so that these officers are taken back to continue with this project after they have been cleared so that we do not lose the funds from the donors. There will be a workshop at Machakos very soon regarding the second phase so that we are in rhyme with the schedule of this programme.

I, therefore, thank the Members, the Whole House, and the Committee for standing with me on this Motion. Let every officer be given the mandate to oversee a project as required. Thank you.

(Question put and agreed to)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

DEFERMENT OF ORDERS NUMBER NINE AND TEN IN TODAY'S ORDER PAPER

The Speaker (Hon.Mwambire): Thank you very much, Members, for your deliberations. Something is appearing in the Order Paper after the Motion we have adopted. We were supposed to have the numbers nine and number ten. Let numbers nine and ten be taken back to the House Business Committee for allocation of time. I thought it was fair for us to have a wider discussion about the Report because the contents were too heavy, and I thought if we did partial engagement, people would not understand because I wanted all Members to get an opportunity to give their views. It was not fair to seek an adjustment of time so that we can deliberate on the two remaining businesses. We can handle them next week probably if the House Business Committee allocates time.

ADJOURNMENT

The Speaker (Hon. Mwambire): The House stands adjourned until Monday next week at 2:30 p.m. May God bless you and have a nice journey Members.

The House rose at 4:23 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*